

TANGAZO LA SERIKALI Na. 539K la tarehe 30/6/2024

**SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)**

KANUNI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 122)

KANUNI ZA UTARATIBU WA KUJIREJESHEA USHURU WA BIDHAA ZA MWAKA 2024

Jina **1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utaratibu wa Kujirejeshea Ushuru wa Bidhaa za mwaka 2024 na zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2024.

Tafsiri **2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 147 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa;
“pombe kali ya ethili” maana yake ni pombe ya ethili asili chini ya namba ya utambuzi wa bidhaa 2207.10.00;
“mzalishaji” maana yake ni mtu aliyepewa leseni ya kutengeneza au kuzalisha bidhaa kwa kutumia pombe kali ya ethili kama malighafi na ameweka mfumo wa stempu za kielektroniki za ushuru wa bidhaa kwa mujibu wa Sheria;
“bidhaa” maana yake ni bidhaa zinazotozwa ushuru chini ya kichwa cha namba ya utambuzi wa bidhaa 22.08 na mvinyo uliochanganywa na pombe kali chini ya kichwa cha namba ya utambuzi wa bidhaa 22.04;
“kipindi cha ushuru” maana yake ni mwezi wa kalenda, unaoanza mwanzoni mwa siku ya kwanza ya mwezi na kuishia siku ya mwisho ya mwezi.

Mazingira ya kujireshea ushuru **3.-(1)** Mzalishaji atakuwa na haki ya kujirejeshea ushuru uliolipwa kwenye pombe kali ya ethili.

(2) Mzalishaji ataruhusiwa kujirejeshea kiasi cha ushuru kilicholipwa kwenye pombe kali ya ethili ikiwa-

(a) pombe kali ya ethili ilinunuliwa kutoka kwa mzalishaji mwenye leseni na ambaye alilipa

ushuru kwenye pombe kali hiyo;

(b) pale ambapo pombe kali ya ethili iliingizwa nchini, mzalishaji alilipa ushuru uliowekwa kwenye pombe kali hiyo wakati wa uingizaji; au

(c) pombe kali ya ethili ilinunuliwa kutoka kwa muingizaji ambaye alilipa ushuru wakati wa uingizaji nchini.

(3) Mzalishaji hataruhusiwa kujirejeshea ushuru uliolipwa kwenye-

(a) bidhaa nyingine isipokuwa pombe kali ya ethili;

(b) huduma;

(c) pombe kali ya ethili iliyoharibiwa, iliyoisha muda wake au iliyoharibika; au

(d) pombe kali ya ethili iliyopotea.

Utaratibu
wa
kujirejeshea
na kulipa
ushuru

4.-(1) Kwa madhumuni ya kujirejeshea, mzalishaji atawasilisha ritani kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 137 cha Sheria kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali.

(2) Kiasi halisi cha ushuru kinachopaswa kulipwa na mzalishaji kwenye bidhaa kitakokotolewa kwa-

(a) kujumlisha ushuru unaopaswa kulipwa na mzalishaji kwenye bidhaa zilizotengenezwa au zilizozalishwa katika kipindi cha ushuru husika; na

(b) kutoa ushuru uliolipwa kwenye pombe kali ya ethili iliyotumika kama malighafi kwenye kutengeneza bidhaa zilizorejelewa katika aya ya (a) katika kipindi cha ushuru husika.

(3) Endapo kiasi halisi cha ushuru katika kipindi cha ushuru husika ni kiasi chanya-

(a) kitahasibiwa na kulipwa na mzalishaji wakati wa uwasilishaji wa ritani; na

(b) wajibu wa kulipa kiasi halisi utatokana na masharti ya kifungu hiki na hautategemea makadirio ya ushuru yaliyofanywa na Kamishna Mkuu.

(4) Endapo kiasi halisi cha ushuru kwenye kipindi cha ushuru husika ni kiasi hasi, kitapelekwa katika vipindi vinavyofuata visivyozidi vipindi sita vya ushuru

vinavyofuatana.

(5)-Endapo kiasi cha ushuru kinachopaswa kulipwa katika kipindi cha ushuru ni sifuri, mzalishaji hatawajibika kulipa ushuru.

Uthibitisho
wa ushuru
uliolipwa na
pombe kali
ya ethili
iliyotumika

5. Mzalishaji hatajirejeshea ushuru uliolipwa kwenye pombe kali ya ethili, isipokuwa kama wakati wa kuwasilisha ritani ya kipindi cha ushuru husika mtengenezaji huyo-

- (a) ikiwa ni pombe kali ya ethili iliyoingizwa nchini na mzalishaji, ana uthibitisho wa malipo ya ushuru, hati ya kutoa mzigo au hati inayofanana na hiyo, yenye jina na nambari ya utambulisho wa mlipakodi ya mzalishaji;
- (b) ikiwa ni pombe kali ya ethili iliyouzwa kwa mzalishaji-
 - (i) na mzalishaji wa pombe kali ya ethili mwenye leseni, ana ankara halali ya kodi au risiti ya mashine ya kielektroniki inayoonesha kiwango halisi kilichonunuliwa;
 - (ii) na muingizaji wa bidhaa nchini aliyepewa leseni, ana ankara halali ya kodi au risiti ya mashine ya kielektroniki inayoonesha kiwango halisi kilichonunuliwa na ushuru husika uliolipwa na muingizaji wakati wa kuingiza mchini inayoonesha namba ya kadhia ya mzigo husika;
- (c) tamko la kiasi cha pombe kali ya ethili iliyotumika na fomula ya uzalishaji iliyotumika kuzalisha au kutengeneza bidhaa katika kipindi husika cha ushuru;
- (d) taarifa ya mfumo wa stempu za kielektroniki inayoonesha kiasi cha bidhaa zilizozalishwa kwa kutumia pombe kali ya ethili katika kipindi husika cha ushuru; na
- (e) taarifa ya usuluhisho wa hesabu endapo kuna tofauti kati ya matokeo yaliyopatikana katika aya (c) na (d).

Ukomo wa
kujirejeshea

6. Mzalishaji hataruhusiwa kujirejeshea ushuru uliolipwa kwenye pombe kali ya ethili baada ya kipindi cha miezi sita kupita kutoka tarehe ya ankara ya kodi, risiti ya mashine ya kielektroniki, hati ya kutoa mzigo au uthibitisho mwingine uliorejewa chini ya kanuni ya 5.

Kanuni Za Utaratibu wa Kujirejeshea Ushuru wa Bidhaa
Tangazo la Serikali Na.539K (Linaendelea.)

Jumla ya Mali iliyotayari kwa uzalishaji (Total stock available for deliveries)

ONDOA: Mali ambayo haikutumika mwishoni mwa mwezi
(Stock on hand at the end of the month)

Mali iliyotumika ndani ya kipindi cha mwezi (Total deliveries during the month)

ONDOA: Punguzo linalotokana na mauzo ya nje (Remission/Rebates on exports
and/or ships store (weka kiambatisho)

ONDOA: Punguzo linalotokana na uharibifu wa mali (Remissions/rebates on
deficiencies allowed by the Commissioner....weka kiambatisho)

Jumla ya Kiasi kilichozalishwa kinachopaswa kulipiwa ushuru
(Total Quantities Liable for Excise Duty)

Kiwango cha Ushuru wa bidhaa kinachohusika
(kama viwango vipo vingi weka kiambatisho)

Jumla ghafi ya Ushuru wa Bidhaa unaopaswa kulipwa
(Total Gross Excise duty payable) SHS

ONDOA: Ushuru uliolipwa wakati wa kununua/kuingiza malighafi ya Ethano
(H.S. CODE 2207.10.00) SHS

Jumla Baki ya Kiasi cha Ushuru wa Bidhaa unaopaswa kulipwa
(Total Net Excise duty payable) SHS

B: TAMKO

Natamka kwamba taarifa nilizojaza kwenye fomu hii pamoja na nyaraka zilizoambatishwa ni sahihi, kamilifu na zinajumuisha kiasi sahihi cha kodi kinachopaswa kulipwaa kwa mujibu wa uelewa na ufahamu wangu.

Jina la Kwanza

Jina la Kati

Jina la mwisho

Nafasi.....

Sahihi.....

Tarehe.....

Dodoma,
30 Juni, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
Waziri wa Fedha